TANGAZO LA SERIKALI Na. 514 la Tarehe 14/9/2018

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA

(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*Zimetungwa chini ya Kifungu vya 6(1) na 16(1)*

SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA MAEGESHO YA MAGARI) ZA HALMASHAURI YA MJI KONDOA ZA MWAKA, 2018

Jina na mwanzo wa kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ushuru wa Maegesho ya Magari) za Halmashauri ya Mji Kondoa za mwaka 2018 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la mamlaka ya Halmashauri ya Mji Kondoa.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakapoelezwa vinginevyo-

*"Afisa Mwidhiniwa"* maana yake ni Afisa yeyote wa Halmashauri aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

*"Chombo cha usafiri"* maana yake ni chombo cha moto ikijumuisha gari au pikipiki zenye magurudumu matatu.

TANGAZO LA SERIKALI Na. 514 la Tarehe 14/9/2018

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA

(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*Zimetungwa chini ya Kifungu vya 6(1) na 16(1)*

SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA MAEGESHO YA MAGARI) ZA HALMASHAURI YA MJI KONDOA ZA MWAKA, 2018

Jina na mwanzo wa kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ushuru wa Maegesho ya Magari) za Halmashauri ya Mji Kondoa za mwaka 2018 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la mamlaka ya Halmashauri ya Mji Kondoa.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakapoelezwa vinginevyo-

*"Afisa Mwidhiniwa"* maana yake ni Afisa yeyote wa Halmashauri aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

*"Chombo cha usafiri"* maana yake ni chombo cha moto ikijumuisha gari au pikipiki zenye magurudumu matatu.

*"Halmashauri"* maana yake ni Halmashauri ya Mji Kondoa

*"Maegesho"* maana yake ni sehemu iliyoainishwa na Halmashauri kwa ajili ya kuegesha chombo cha usafiri isipokua stendi.

*"Maegesho maalum"* maana yake ni eneo lililotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuegesha chombo cha usafiri kwa utaratibu uliowekwa kwenye kifungu cha 8 cha Sheria Ndogo hizi.

*"Mkurugenzi"* maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Kondoa pamoja na Afisa yeyote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi.

*"Yadi"* maana yake ni eneo lililotengwa kwa ajili ya kuhifadhi vyombo vya usafiri.

*"Ushuru wa Maegesho"* maana yake ni Ushuru unaotozwa na Halmashauri kwa mtu yeyote anaye egesha chombo cha usafiri katika eneo lililoainishwa na Halmashauri.

Mamlaka ya Halmashauri

4. (1) Halmashauri itatenga maeneo ya maegesho kwa vyombo vya usafiri vitakavyoegeshwa katika maeneo yaliyoainishwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

(2) Halmashauri itatoza Ushuru wa maegesho kwa mujibu wa viwango vilivyoainishwa katika Jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hizi.

Sehemu ya maegesho

5\. (1) Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi maeneo yote yaliyoainishwa katikati ya Mji yatakuwa ni sehemu za maegesho ya vyombo vya usafiri

(2) Itakua ni wajibu kwa mtu yeyote kuegesha chombo cha usafiri katika eneo lililoainishwa na Halmashauri.

Namna ya kutoza Ushuru wa maegesho

6\. (1) Ushuru wa Maegesho utatozwa kuanzia saa 12:00 asubuhi hadi saa 12:00 jioni kila siku.

(2) Ushuru wa maegesho utalipwa kwa kila siku au mwezi kadri Halmashauri itakavyoona inafaa.

(3) Ushuru wa maegesho utalipwa na mtu yeyote mara tu anapoegesha chombo cha usafiri.

(4) Endapo mtu yeyote amelipa ushuru wa maegesho kwa siku au kwa mwezi ataruhusiwa kuegesha chombo cha usafiri alicholipia katika eneo lolote lililoainishwa kwa ajili ya maegesho ndani ya Halmashauri kwa muda aliolipia.

(5) Bila kuathiri kifungu kidogo cha (3) cha kifungu cha 6 cha Sheria Ndogo hizi, chombo cha usafiri kinachomilikiwa na Serikali, wanadiplomasia, Majeshi, na magari ya kubeba wagonjwa hayatatozwa ushuru wa maegesho.

Mamlaka ya Halmashauri

7\. (1) Afisa Mwidhiniwa atakuwa na mamlaka ya kukamata na kuondoa chombo cha usafiri kilichoegeshwa kwenye eneo ambalo halikuainishwa katika Sheria Ndogo hizi.

(2) Chombo cha usafiri kilichokamatwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1) cha kifungu cha 7 kitaondolewa na kuhifadhiwa katika yadi ya Halmashauri au eneo lililoainishwa na Halmashauri.

(3) Halmashauri itakua na mamlaka ya kuuuza chombo cha usafiri endapo mmiliki wa chombo hicho atashindwa kulipa gharama za kuondoa chombo cha usafiri ndani ya kipindi cha siku kumi na nne (14) tangu tarehe ya kukamatwa.

Maegesho maalum

8. (1) Halmashauri inaweza kutenga eneo maalum la maegesho ya chombo cha usafiri na kiwango cha ushuru wa maegesho kitakuwa kama ilivyoainishwa kwenye jedwali la pili la Sheria Ndogo hizi.

(2) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu cha 6 cha Sheria ndogo hizi, muda wa kuegesha chombo cha usafiri katika maegesho maalum utapangwa kadri Halmashauri itakavyoona inafaa.

(3) Katika maeneo ambayo hayataruhusiwa kupaki kwa magari Halmashauri itaweka vibao vitakavyozuia maegesho ya magari.

Wajibu kwa Halmashauri wa kulipa fidia

9. Halmashauri itakuwa na wajibu wa kulipa fidia ya hasara itakayosababishwa na Afisa Mwidhiniwa au Afisa yeyote kwa uzembe au makusudi wakati anatekeleza Sheria Ndogo hizi.

Makosa

10. Itakua ni kosa kwa mtu yeyote endapo;-

a) Atashindwa kulipa ushuru wa maegesho;

b) Atamshawishi mtu au kundi la watu kutolipa Ushuru wa maegesho;

c) Ataegesha chombo cha usafiri katika eneo ambalo halijaainishwa na Halmashauri;

d) Ataosha au kufanya matengenezo ya chombo cha usafiri katika eneo la maegesho,

Kufifilisha kosa

11. Mkurugenzi anaweza kumtoza mtu yeyote faini isiyopungua shilingi laki mbili (Tsh.200,000/=) na isiyozidi shilingi laki tano (Tshs. 500,000/=) iwapo mkosaji atakiri kosa kwa maandishi na kukubali kutekeleza wajibu wake pamoja na kulipa faini anayodaiwa kama itakavyoelekezwa kwenye jedwali la tatu la Sheria Ndogo hizi.

Adhabu

12. Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi laki mbili (200,000/= na isiyozidi shilingi milioni moja (1,000,000/=) au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili (12) jela na kisichozidi miaka miwili (2) jela au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

JEDWALI LA KWANZA

USHURU WA MAEGESHO

(Limetungwa Chini ya Kifungu cha 4(2))

Viwango vya Ushuru wa Maegesho.

| Na. | AINA YA CHOMBO CHA USAFIRI | KIASI CHA USHURU KWA SIKU | ENEO LILILOTENGWA |
|---|---|---|---|
| 1. | Gari ya mizigo,basi na pickup kubwa zaidi ya tani 7 | Tsh.1,000/= | BICHA |
| 2. | Gari ya mizigo/basi/pick up chini ya tani 7 | Tsh.500/= | BICHA |
| 3. | Teksi | Tsh.500/= | BICHA |
| 4. | Pickup/Station wagon | Tsh.1,000/= | BICHA |
| 5. | Pikipiki ya magurudumu mawili iliyosajiliwa kwa biashara | Ths.300/= | BICHA |
| 6. | Pikipiki ya magurudumu matatu | Tsh.500/= | BICHA |
| 7. | Magari mengine yasiyo ya biashara | Tsh.500/= | BICHA |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 8. | Faini ya kupaki maeneo yasiyoruhusiwa | Tsh.50,000/= | KWAPAKACHA |
| 9. | Gharama za kukokota gari lililotelekezwa | Tsh.30,000/= | KWAPAKACHA |
| 10 | Faini ya kutunza gari chini ya tani 7 lililotelekezwa kwenye uzio wa Halmashauri (yard) | Tsh.10,000/= | KWAPAKACHA |
| 11 | Faini ya kutunza gari zaidi ya tani 7 lililotelekezwa kwenye uzio wa Halmashauri (yard) | Tsh.20,000/= | KWAPAKACHA |

JEDWALI LA PILI

VIWANGO VYA USHURU WA MAEGESHO MAENEO MAALUM

*(Limetungwa Chini ya Kifungu cha 8(1))*

| Na. | AINA YA CHOMBO CHA USAFIRI | KIASI CHA USHURU KWA SIKU | ENEO LILILOTENGWA |
|---|---|---|---|
| 1. | Magari makubwa | Tsh 2,500/= kwa masaa kumi na mbili | KWAPAKACHA |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 2. | Magari madogo | Tsh 2,500/= kwa masaa kumi na mbili | KWAPAKACHA |

JEDWALI LA TATU

HATI YA KUFIFILISHA KOSA

*(Limetungwa Chini ya Kifungu cha 11)*

Mimi ........................................ nakiri kwa hiari Yangu Mwenyewe mbele ya…………………...... ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Kondoa kwamba mnamo tarehe …….. Mwezi ……….......... Mwaka ............ nilitenda kosa la kukiuka masharti ya Sheria Ndogo za Ushuru wa Maegesho za Halmashauri ya Mji wa Kondoa za Mwaka 2018.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri niko tayari kulipa kiasi cha Ushuru wa Maegesho ninaodaiwa pamoja na faini.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe .....................ya Mwezi ...........Mwaka 2018

Jina: ............................................

Saini: ...........................................

Mbele ya: ....................................

Cheo: ...........................................

Saini: ...........................................

Tarehe: ........................................

Nembo ya Halmashauri ya Mji wa kondoa imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Halmashauri uliofanyika tarehe 13/5/2017 mbele ya:-

KHALIFA KONDO
*Mkurugenzi wa Mji*
*Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa*

L.S

HAMZA MAFITA
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa*

NAKUBALI,

DODOMA,
15 Agosti, 2018

SELEMANI S. JAFO (MB.),
*Waziri wa Nchi-OR-TAMISEMI*